

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

632

SAYANSI

Muda: Saa 3

Ijumaa, 10 Mei 2019 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na **maswali (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



1



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Orodhesha vyanzo vinne vya ajali ya moto shuleni na katika mazingira ya nyumbani.
2. Kwa ufupi, bainisha matumizi manne ya mashine za roda katika maisha ya kila siku.
3. Kwa kutoa hoja moja kwa kila homoni, eleza kwa ufupi madhara ya kutolewa kwa kiwango kikubwa kwa homoni zifuatazo katika mwili wa binadamu:
 - (a) Thairoksini
 - (b) Adrenali
 - (c) Insulin
 - (d) Oestrojeni.
4. Kwa kutoa mifano, bainisha mambo manne uliyojifunza katika darasa la Sayansi na yanaonekana katika maisha ya kila siku.
5.
 - (a) Orodhesha tabia mbili za maada katika hali ya kimiminika.
 - (b) Kwa kutoa mifano, taja chembechembe ndogo tatu zinazounda maada.
6. Kwanini ni lazima walimu waandae azimio la kazi kabla ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji? Toa hoja nne.
7. Orodhesha visababishi vinne vya magonjwa yasiyoambukiza.
8. Taja sifa tatu za nishati ya sauti na pendekeza njia moja ya kuzuia mwangwi usitokee.
9.
 - (a) Taja mbinu nne zinazotumika kupima maendeleo ya wanafunzi katika somo la Sayansi.
 - (b) Orodhesha mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa mazoezi ya darasani.
10.
 - (a) Taja vitu viwili visivyo hai vinavyohitajika kwa ukuaji wa mmea.
 - (b) Kwa kutoa hoja tatu, eleza kwa ufupi ni namna gani binadamu hutegemea mimea katika kuishi.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (02)** kutoka sehemu hii.

11.
 - (a) Fafanua vyanzo vitano vya umeme unaotumika katika maisha ya kila siku.
 - (b) Kwa kutumia michoro, eleza kanuni mbili za ncha za sumaku.

12. Kwa kutoa mifano, bainisha aina sita za mashine rahisi zinazotumika katika maisha ya kila siku.
13. Fafanua kasoro tatu zinazoweza kujitokeza katika mfumo wa uzazi wa mwanamke na mwanaume na kusababisha ugumba.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (02) kutoka sehemu hii.

14. (a) Nini maana ya shajala ya somo? Kwa kutumia jedwali, oneshwa muundo na vipengele vilivyomo kwenye shajala ya somo la Sayansi.
(b) Bainisha umuhimu wa shajala ya somo la Sayansi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Toa hoja tatu.
15. Eleza tahadhari sita za kuchukua unapofanya kazi katika chumba cha maabara ya Sayansi.
16. Fafanua hatua za kufuata katika kufundisha somo la Sayansi kwa kutumia mbinu ya changanyakete na matembezi ya galari.